

**TAARIFA KWA NAIBU WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS MUUNGANO NA
MAZINGIRA MHESHIMIWA MUSSA SIMA (Mb.) KUHUSU UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA
USIMAMIZI WA MAZINGIRA KATIKA WILAYA YA MPWAPWA TAREHE 14/08/2018**

1. UTANGULIZI

Mhe. Naibu Waziri wa nchi ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira,
Wilaya ya Mpwapwa ni kati ya Wilaya nane (8) za Mkoa wa Dodoma. Wilaya ya Mpwapwa inapakana na wilaya ya Kongwa Kwa upande wa kaskazini, Wilaya ya Chamwino Kwa upande wa Magharibi, Upande wa mashariki inapakana na Wilaya ya Kilosa na Upande wa kusini inapakana na Wilaya ya Iringa.

Mhe. Naibu Waziri,

Wilaya ya Mpwapwa ina ukubwa wa eneo la kilometa za mraba 7,479 sawa na asilimia 18.35 ya eneo lote la Mkoa wote wa Dodoma. Eneo hili ambalo ni sawa na hekta 737,900 linatumika kwa shughuli za kilimo(228,991hk), ufugaji(262,000) , hifadhi ya misitu(53,122.28hk) pori tengefu(136,450 hk) Bwawa (64,000hk na Makazi (30,928 hk)

2. USIMAMIZI NA UHIFADHI WA MAZINGIRA

Mhe. Naibu Waziri,

Mazingira ni kila kitu kinachomzunguka binadamu hivyo basi kwa mujibu wa **sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 kifungu 4 (1) na (2)**, kila mtu ana haki ya kuishi katika mazingira safi na salama ikijumuisha haki ya kupata na kutumia sehemu za jamii na za mazingira kwa ajili ya kujiliwaza, elimu, afya, kiroho, kitamaduni na kiuchumi.

Mhe. Naibu Waziri,

Hali ya uhifadhi wa Misitu na mazingira kwa ujumla katika Wilaya ya Mpwapwa ni ya wastani kwani jamii bado inafanya shughuli mbalimbali zinazopelekea uvamizi wa misitu na uharibifu wa mazingira kama uchomaji wa mkaa, ufugaji usiokua na tija, kilimo holela, uchimbaji wa madini holela, ukataji wa miti kwa matumizi mbalimbali kama ujenzi na nishati, Aidha zipo baadhi ya kata ambazo zina uharibifu mkubwa wa mazingira hasa ikolojia ya milima na uvamizi wa vyanzo vya maji . kata hizo ni pamoja na kata ya Mazae, N'ghambi, Mpwapwa mjini, Rudi, Wotta, Malolo, Chitemo, Galigali, Ipera, Mang'haliza, Mbuga na Rufu.

Mhe. Naibu Waziri,

Mazae ni kati ya kata zinazozunguka mlima wa kiboriani ambao ni sehemu ya safu za ikolojia ya milima Rubeho ambao ni chanzo kikubwa cha maji katika wilaya ya Mpwapwa na vijiji vyake, Aidha eneo hili ni muhimu sana kwa wakazi wa Mpwapwa na Kongwa kwani ndipo huduma nyingi za ikolojia hupatikana kwa ajili ya uhai wa viumbe wote ikiwemo binadamu. Pamoja na faida hizo wanachi wa mazae na wananchi kutoka kata nyingine hata nje ya wilaya wamekuwa wakifanya uharibifu mkubwa wa mazingira na vyanzo vya maji aidha kwa kujua au kutokujua kiasi kwamba uharibifu huu wa safu za mlima kiboriani umekuwa tishio kwa Maisha ya viumbe, makazi na maendeleo ya Makao makuu ya Mji wa Mpwapwa ambao kwasasa unakabiliwa na uwepo wa makorongo Makubwa ikiwemo korogo linalopita katikati ya Mji wa Mpwapwa.

3. VISABABISHI VYA UHARIBIFU WA MISITU NA MAZINGIRA

Mhe. Naibu Waziri,

Mojawapo ya sababu kubwa za uharibifu wa mazingira na vyanzo vya maji ndani ya Wilaya ni pamoja na uchomaji mkaa, kilimo na ufugaji holela, uchimbaji wa madini holela, ukosefu wa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji, siasa hasa nyakati za uchaguzi, uwindaji, ongezeko la watu ambao hutafuta miti kwa ajili ya kujengea makazi yao na kuanzisha mashamba mapya, kutozingatia sheria zilizopo kuhusu usimamizi wa misitu, na uelewa mdogo kuhusu umuhimu wa misitu.

4. JUHUDI KATIKA KUDHIBITI UHARIBIFU WA MISITU NA MAZINGIRA.

Mhe. Naibu Waziri,

Hatua mbali mbali zimekuwa zikichukuliwa kuzuia uharibifu huu na kuhifadhi mazingira na misitu hatua hizo ni pamoja

- ✓ Kutunga sheria ndogo (By-law) za Halmashauri zinazohusu uhifadhi wa mazingira
- ✓ Kuhuwisha kamati za mazingira za wilaya, Tarafa, Kata, na Vijiji ambazo kiujumla zimekuwa zikifanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha lengo la usimamizi na uhifadhi wa mazingira linatekelezwa kwa ufasaha.
- ✓ Kufanya doria mbali mbali kwenye vijiji, milimani na maeneo ya hifadhi na kubainisha na kuorodhesha uharibifu wote wa mazingira na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria ikiwemo mahakamani ambapo 2016 – Agosti, 2018 zaidi ya

watuhumiwa 50 waharibifu wa mazingira walikamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria, Watuhumiwa 12 kutoka kata ya Maze kati yao 6 walifungwa miaka miwili na kisha vifungo vyao kubadilishwa na kuwa vifungo vya nje.

- ✓ Utoaji wa elimu na uhamasishaji wa shughuli za uhifadhi wa mazingira ikiwemo upandaji Miti ambapo mwaka 2017/2018 Wilaya ya Mpwapwa ilipanda Miti 812,328 kati ya lengo la 1,500,000 pia tayari tunavyo vikundi zaidi ya 3 vya uhifadhi wa mazingira ikiwemo kikundi cha Jipemoyo kutoka kitongoji cha Kiboriani ambacho kwa namna ya pekee kwa mwaka 2017/2018 kimepanda miti aina ya pain 11,225.
- ✓ Halmashauri imeainisha vyanzo vya maji na baadhi ya vyanzo hivyo vimewekwa mipaka ya umbali wa mita 60 katika Kata za Rufu na Pwaga , sambamba na hilo watuhumiwa 24 kutoka Kitongoji cha Kiboriani wamefikishwa Polisi ili hatimaye wafikishwe kwenye vyombo vya sheria.

Mhe. Naibu Waziri,

Mojawapo ya nyenzo ambazo hutumika katika kupunguza, kufuatilia na kukabiliana na Athari hizi za kimazingira katika Wilaya ya Mpwapwa ni pamoja na Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIA) ndani ya **Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 Kifungu 81(1)**, Mpango wa Usimamizi wa Mazingira ndani ya **Kanuni za Ukaguzi na Tathmini ya Athari kwa Mazingira 2005 kutoka kifungu 82(1) and 230 (2) (h) na (q) cha Sheria ya Mazingira** pamoja na nyinginezo zinazotambulika kisheria.

5. CHANGAMOTO

Mhe. Naibu Waziri,

Pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na uongozi wa Wilaya, wadau na Wananchi katika suala hili la uhifadhi wa mazingira bado zipo changamoto zinazo tukabili ili kufikia malengo kwa ufanisi. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo;

- Upungufu wa maafisa usimamizi wa mazingira wenye weledi katika ngazi za Wilaya kata na vijiji ambapo ngazi ya wilaya Afisa usimamizi wa Mazingira kwa sasa yuko 1 na ngazi zingine hakuna kabisa.
- Bajeti finyu kwaajili ya shughuli za uhifadhi wa mazingira
- Ukosefu wa vitendea kazi (usafiri NK)
- Mwingiliano wa Siasa zisizo na tija katika kuhifadhi na kulinda mazingira
- Adhabu ndogo kwa waharibifu wa mazingira wanapofikishwa mahakamani

- Uelewa mdogo wa wananchi na mazoea kuhusu uhifadhi na ulinzi wa mazingira
- Mabadiliko ya tabianchi

6. MAPENDEKEZO/UTATUZI WA CHANGAMOTO

- Wizara ya Muungano na Mazingira ione namna ambavyo inaweza kuwasiliana na OR- TAMISEMI na kuishauri kuajiri maafisa wasimamizi wa mazingira au kuandaa muongozo wa namna ya kufundisha maafisa wasimamizi wasaidizi wa mazingira ngazi ya kijiji na kuwaajili ili kuimarisha usimamizi na uhifadhi wa mazingira katika nchi yetu.
- Wizara ya Muungano na Mazingira iandae utaratibu wa kusaidia bajeti au uanzishaji wa miradi kwaajili ya shughuli za uhifadhi wa mazingira ikiwemo kampeni ya kitaifa ya upandaji miti 1,500,000 kwa kila Wilaya.
- Wizara ya Muungano na Mazingira isaidie upatikanaji wa vitendea kazi kwa maafisa mazingira ngazi ya Halmashauri hasa usafiri ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kwa wakati.
- Wanasiasa wasiwe sehemu ya kushawishi wananchi kuharibu mazingira bali wawe sehemu ya wachukua hatua dhidi ya waharibifu wa mazingira katika maeneo yao ya kiutawala .
- Agenda ya uhifadhi wa mazingira kwa Taifa iwe ni agenda ya kudumu na endelevu kwa ngazi zote za uongozi na vikao vyote ili tuweze kufikia lengo la kuwa na uhifadhi wa mazingira endelevu kwa Tanzania ya viwanda.

Mhe.Naibu Waziri,

Naomba kuwasilisha.

Maria P. Leshalu

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)

Mpwapwa